# Kila Raia Aipende Nchi Yake



*Hayati Mzee Jomo Kenyatta, Rais wa Kwanza wa Taifa la Kenya.*

WAKENYA WASHEREHEKEA Siku Kuu ya Kenyatta. Hino ni ya kumi na nane tokea kunyakua Uhuru toka kwa Wakoloni. Hii ni siku ya kukumbusha wapigania uhuru wa nchi ya Kenya. Wote wale ambao walijitolea kwa damu, mali, jasho na mawazo hadi uhuru ukanyakuliwa. Waliopigana misituni na pia wale waliokuwa wakiwatibu majeruhi na kuwaandalia vyakula wote wastahiki sifa ya ushujaa. Na twafahamu kwamba Jemedari Mkuu wa vita hivyo vya kimwili na vya kimawazo si mwengine ila ni Marehemu Mzee Jomo Kenyatta mwanzilishi wa Taifa huru la Kenya. Leo hatuna budi kumuombea Mungu amrehemu katika malazi yake.

Hatusahau vile Mzee Kenyatta alivyoanzisha taifa huru. Yaani raia pamoja na wakazi wote wa nchi hii wakijifanyia biashara zao, kulima makonde yao, kujenga miji yao na kuabudu dini zao bila ya kuingiliwa na serikali bora tu iwe katika mambo yao hayo wanafata sheria za nchi hii. Na mara tu kuondoka kwa Mzee Kenyatta, alitawala Bwana Daniel Arap Moi ambaye maneno yake ya kwanza ni kuwa atafata Nyayo za Kenyatta. Na kwa kweli hivyo ndivyo mambo yalivyo. Kwani uhuru wa kutembea, kusema, kufanya biashara na kuabudu mpaka dakika hii unalindwa na katiba ya Kenya.

Si hayo tu bali Rais Moi alikuja na hamu kubwa ya kuendelea kudumisha amani, utulivu na upendo. Hayo ni mambo ambayo Rais asema kwamba ndio msingi wa maisha ya wanadamu. Na pia ni sifa ambazo hutazamwa na mataifa mengine ambayo yangependa kuja kushirikiana na Kenya kwa biashara, uchumi na utamaduni. Hivyo basi serikali ya Kenya chini ya uongozi wa busara wa Rais Moi haikubakisha hata hatua moja kuichukua ili kuhakikisha kwamba nchi hii itadumu na amani. Na ndipo katika risala yake ya Siku kuu hii, Rais akaita mwito wa kupenda nchi yako.


Kuipenda nchi yako, ni pamoja na kufata sharia za nchi. Umuangalie kila mtu kama Mkenya wala usimuangalie kwa kabila yake ama rangi yake. Kwani kila raia wa nchi hii ana haki sawa sawa na kila raia mwengine. Na kuipenda nchi yako ni kuwapenda raia wenzako kama ujipendavyo wewe mwenyewe. Jambo jengine ambalo Rais Moi hulitilia sana maanani kwa maslaha ya nchi hii, ni vile kila wakati kuwahimiza watu wafikirie wenzao. Hasa hapa huhusika zaidi raia ambao wana madaraka ya kazi, fedha ama mapato. Kwa kifupi tu, ikiwa wewe unamfikiria raia mwenzako kwamba na yeye pia anataka apate riziki yake na watoto wake, huwezi kufanya njama za kutorosha chakula toka nchi hii hadi ya jirani kwa shebaha ya kujipatia utajiri wa haraka na ilhali wajua kwamba kuna maelfu ya raia ambao wanakihitaji chakula hicho.

Wakenya wote ni budi kushirikiana na serikali ili tudumishe amani na kusaidia ndugu zetu ili sote tuishi kama Wakenya katika Kenya huru.




*KAMPUNI YA KBS hivi karibuni iliandaa karamu Nyali Beach Hotel kumwaga Meneja Mkuu Bw. Jack Steadman ambae amestaafu baada ya miaka 28 kazini. Pichani anaonekana mwenyekiti wa K.B.S. Bw. Clymo, Bi. Mollie Steadman, Meneja mpya Bw. Lutaf Maherali, na Bw. Steadman.*

PICHA: MWAKINA



*HII NI harusi iliyofana sana iliyofanyika Mombasa Memorial Cathedral kati ya Bw. Morriee N. Kioko mfanyi kazi wa Law Courts Mombasa na Bi. Rachel Kasana kutoka mabule kilamatinde*




**MTUKUFU Rais Daniel Arap Moi ambaye katika sherehe za Kenyatta Day aliwahimiza wananchi kujizatiti na kulinda Uhuru wa nchi yao tukufu ya Kenya.**

# Musiharibu Dini Kwa Kuiga

NIMESIKITISHWA sana kusoma katika *COASTWEEK* ya October 2.10.1981 Sauti ya wasomaji ubishi wa bibi Zaituni Said Mohammed kuhusu kuiga mila za kikristo katika sherehe za harusi za Kiislamu, bibi huyo alitaka aambiwe katika kifungu gani cha Biblia au Kurani kinacho eleza kwamba veli ni vazi la kikristo ningependa kumjibu bibi huyo ya kwamba hakuna kifungu chochote katika Kurani wala Biblia kinachoeleza hivyo.

Lakini ningependa kumjulisha kwamba veli, mishumaa na kuvalishana pete hadharani ni mila katika mila za kikristo, na si lazima ziwe zimeandikwa katika Biblia au Kurani au kitabu chochote kingine.

Katika Kurani Mwenyezi Mungu anasema katika Surat -al-Baqara 120 "Hawatakuwa Radhi juu yako Mayahudi wala Wakristo mpaka ufuate Mila yao." Kwa hivyo bibi mfano wa Zaituni afaa azingatie maneno haya ya Mwenyezi Mungu na kuachiliambali uigaji wa mila za Kikristo.

Mwisho ningependa kumkumbusha Zaituni msemo mmoja wa Kiswahili usemao "Mwacha asili ni mtumwa".

**Abbasi B. Mohammed,**
**MOMBASA.**

*Mjadala huu umefungwa.*
*— MHARIRI*

## *SAUTI ZA WASOMAJI*

**COASTWEEK** Sanduku La Posta 87270, Mombasa KENYA

# *ENEZENI MAOFISI*

KUHUSU shindano la Kujaza Swahili Crossword, jambo la kushangaza ni kwamba utaona imeandikwa "Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*".

Ninge penda kuuliza neno moja, je mshindi yeyote kutoka Nairobi, Kisumu, Lamu etc, etc. itambidi asafiri hadi Mombasa kwa ajili ya hiyo zawadi ya miavuli? Inge kuwa bora ikiwa *COASTWEEK* wange kuwa na branch yao kila miji ili washindi wasiwe na haja ya kusafiri hadi Mombasa. Je wasomaji ni sawa?

**Anwar M. K.**
**MOMBASA.**
*Pendekezo lako litafikiriwa.*
**MHARIRI.**

☆






*VIFUJO na hoi hoi za harusi zitasikika hapo ifikapo tarehe 31 Oktoba wiki ijayo wakati Bw. Raphael Alex Kea wa Jadini Beach Hotel na Bi. Beatrice K. Samuel bintiye Bw. Samuel Kazungu watakapo zifunga pingu za maisha katika kanisa la Makupa. Baadaye kutakua na tafrija ya mwaka vyumbani mwa Bwana Arusi nyumbani kwake Malindi ambayo itahudhuriwa na wageni mashuhuri kutoka Mombasa na Nairobi na kutumbuizwa na wana boma liwanza kutoka Nairobi.*

# JISHINDIE
## Miavuli maridadi katika shindano jipya la kujaza maneno






## *SWAHILI CROSSWORD NO. 129*

*KWENDA KULIA:*

1. Sehemu iliyo na nafasi katika nyumba.
4. Ufupi wa bibi
5. Kivazi cha kike
7. Sehemu karibu ya shingo
8. Ama
9. Upwa
12. Ndege mwenye thamani
13. Kiungo cha maneno
14. Sehemu ya mbele ya chombo
15. Toa moshi kwa kinga
17. Sehemu moja ya kumi ya mia
18. Ala, jalada

*KWENDA CHINI:*

1. Chakula kilicho ungua chini ya sufuria au chungu
2. Mtego wa samaki
3. Kama theluji
4. Sima ya makopa
6. Bora, nzuri zaidi
9. Hutengenezewa mito na magodoro
10. Aina ya majani
11. Jina la Kijaluo
12. Chombo cha nyumbani
16. Neno la kumaka

JINA ............................................

SANDUKU LA POSTA ................................

....................................................

**Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 128**

1] Soody Njjamah, Sanduku la Posta 95712, Mombasa

2] Mrs. Nereya Oremo, Sanduku la Posta 33, Taveta

3] Mr. Petro M. Juma, Sanduku la Posta 30091, Nairobi.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 128 —**

*KWENDA KULIA:*

1. MNYAPARA, 5. SA, 6. KIBABA, 7. LULU, 9. NAWA, 11. INI, 14. LAUMU, 15. NI, 16. LA, 17. PARAGA.

*KWENDA CHINI:*

1. MAKINDU, 2. ALAMA, 3. AWALI, 4. ASALI, 8. UNGUZA, 10. WALI, 12. VUNA, 13. TEMA, 15. NA.

**Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:**

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindi watatu kila baada ya wiki mbili watapata miavuli maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LIMITED*, Mombasa.

Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa Muharirí, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatano terehe 14.11.81 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.